Date Printed: 04/23/2009

| | |
|---|---|
| JTS Box Number: | IFES_73 |
| Tab Number: | 8 |
| Document Title: | Maelekezo Kwa Mpiga Kura |
| Document Date: | 1995 |
| Document Country: | Tanzania |
| Document Language: | Swahili |
| IFES ID: | CE01893 |

*2322FA09-4008-4A6F-BA38-62EFFB5402D8*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MAELEKEZO KWA MPIGA KURA

UCHAGUZI

WA

RAIS NA WABUNGE

1995

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MAELEKEZO KWA MPIGA KURA

## UCHAGUZI

## WA

## RAIS NA WABUNGE

## 1995

# UJUMBE WA MWENYEKITI

Tanzania ni Nchi inayofuata utaratibu wa Vyama vingi vya Siasa. Vyama vinavyoshiriki katika Uchaguzi ni vyama vilivyoandikishwa kisheria, kwa hiyo vinashiriki katika Uchaguzi huu kihalali kabisa.

Kila raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea ana haki ya kujiandikisha kuwa mpiga kura. Kukosa kupiga kura ni kujinyima haki yako. Kwa hiyo una wajibu wa kujiandikisha na kupiga kura. Jiandikishe na kupiga kura hata kama wewe si mwanachama wa chama chochote cha siasa. Kura yako ni siri yako.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inafanya kila linalowezekana ili uchaguzi uwe huru na wa haki.

## USIKOSE KUJIANDIKISHA

## USIKOSE KUPIGA KURA

(Jaji Lewis M. Makame)
**MWENYEKITI**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# UTANGULIZI

Kiti cha Rais/Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kitagombewa na wagombea watakaoteuliwa na Vyama vya Siasa vilivyopata usajili kamili. Mgombea atakayeshinda ndiye atatangazwa rasmi kuwa Rais/Makamu wa Rais kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Kiti cha Ubunge kitagombewa na wagombea wa vyama mbalimbali vya siasa. Mgombea atakayeshinda atakuwa ni Mbunge wa Jimbo lako kwa kipindi cha miaka mitano. Mbunge huyo ndiye atakaye kuwakilisha Bungeni wewe na wenzako wa Jimbo lako.

Kushiriki kwako katika chaguzi hizo ni muhimu kwako na kwa Taifa. Kutokana na umuhimu huu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa Maelekezo haya ili kukusaidia wewe na wenzako kushiriki vyema katika hatua mbalimbali za uchaguzi.

Ni matumaini yangu kwamba Maelekezo haya utayasoma na kuyazingatia.

**UKISHA KUJIANDIKISHA USIKOSE KUPIGA KURA.**

(ALEX T. BANZI)
MKURUGENZI WA UCHAGUZI

## KWA NINI TUNACHAGUA:

- Tunatumia haki yetu Kikatiba.

- Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – ni Wakuu wa Nchi.

- Wabunge ndio wawakilishi wa wananchi Bungeni. Viongozi hao ni muhimu kwa kuwa ndio:-

    - Wanaohamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo yao.

    - Wanaopitisha Sheria na Sera mbali mbali kwa maendeleo ya wananchi.

## KUJIANDIKISHA KUPIGA KURA

## KWA NINI NI MUHIMU KUJIANDIKISHA:

- Bila kujiandikisha hutaruhusiwa kupiga kura.

- Usipopiga kura utakuwa umepoteza haki yako ya kumchagua kiongozi anayefaa.

## LINI UKAJIANDIKISHE:

- Kwa jumla tarehe za uandikishaji wa Wapiga kura hupangwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

- Kwa uchaguzi wa Rais/Makamu wa Rais na Wabunge wa Mwaka 1995 uandikishaji utafanyika kuanzia tarehe 6 Agosti hadi tarehe 4 Septemba, 1995

## WAPI UKAJIANDIKISHE:

- Ukajiandikishe katika kituo cha kujiandikisha kilichopo katika kijiji chako, au Kitongoji chako au Mtaa wako.
- Vituo hivyo vitatangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo lako kabla ya tarehe ya kuanza kujiandikisha.
- Kila mahali pa kujiandikisha patakuwa na bango lililoandikwa **"KITUO CHA KUANDIKISHA WAPIGA KURA".**

## MASWALI UTAKAYOULIZWA WAKATI WA KUANDIKISHWA

Ili uweze kuandikishwa Mwandishi atahitaji kufahamu, kutoka kwako, mambo yafuatayo:

- Majina yako (Jina lako, la baba yako na la ukoo).
- Uraia wako.
  * Kama wewe ni raia wa kuandikishwa, kumbuka namba yako ya kuandikishwa kuwa raia wa Tanzania.
- Umri wako.
- Mahali unapoishi, kwa kawaida.
- Kama hujaandikishwa mahali pengine popote.

**KUMBUKA KUWA TAARIFA SAHIHI NI MUHIMU ILI UWEZE KUANDIKISHWA KUWA MPIGA KURA**

## BAADA YA KUANDIKISHWA:

- Utapewa Fomu Namba 1.

    * Ni Fomu ya Kuandikishwa kuwa Mpiga Kura. Ina namba ya kuandikishwa na tarehe uliyoandikishwa katika Jimbo linalohusika.

    * Itunze vizuri fomu hiyo. Maana ni ushahidi kwamba umeandikishwa . Siku ya kupiga kura **LAZIMA** uende nayo kituoni.

    * Utapewa pia karatasi yenye vidokezo muhimu kuhusu hatua mbalimbali za uchaguzi wa Rais/Makamu wa Rais na Wabunge. Kaisome vizuri.

## UKIKATALIWA KUANDIKISHWA

* Utaelezwa sababu.

* Ukiridhika, rudi nyumbani.

  Usiporidhika, una haki ya kumwomba Mwandishi akueleze sababu hizo kwa maandishi.

* Kama bado huridhiki unaweza kumwona Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au hata Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo lako.

* Kama uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi nao hautakuridhisha una haki ya kwenda kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi. Lakini: itabidi uende kabla ya kupita siku 21 tangu siku utakapokataliwa kuandikishwa.

## FOMU NA. 2 - ORODHA YA WAPIGA KURA WALIOANDIKISHWA:

* Itakuwepo ofisini kwa Msimamizi wa Uchaguzi mara baada ya siku ya mwisho ya uandikishaji wa wapiga kura.

* Una haki ya kukagua orodha hiyo katika kipindi rasmi kitakachowekwa.

* Ukiona jina la mtu ambae una hakika amekufa au hana sifa za kuandikishwa, una haki ya kudai jina hilo lifutwe.

* Ukiona jina lako halimo na una hakika ulijiandikisha una haki ya kudai jina lako liingizwe kwenye orodha hiyo.

## SIFA ZA KUWA MPIGA KURA

- Kuwa raia wa Tanzania.

- Kuwa na umri wa miaka 18 na kuendelea.

- Kuwa mkazi wa kawaida wa eneo unapokuja kujiandikisha kuwa mpiga kura.

## LAKINI

* Hata kama mtu ana sifa hizo zilizotajwa hapo Juu, hastahili kuandikishwa iwapo:

    - ni raia wa nchi nyingine.

    - amethibitishwa kisheria kwamba ni mgonjwa wa akili, ni mwendawazimu na amewekwa kizuizini kwa ajili hiyo.

    - amewekwa kizuizini kwa amri ya Rais

    - amehukumiwa kifo au anatumikia kifungo kinachozidi miezi sita.

- kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge inayoshughulikia makosa yanayohusika na uchaguzi wa aina yoyote mtu huyo amezuiliwa kujiandikisha kama mpiga kura.

## UTEUZI WA WAGOMBEA

### (i) WAGOMBEA URAIS NA MAKAMU WA RAIS

* Sharti wateuliwe na vyama vyao vya siasa.

* Pia sharti wateuliwe na watu 200 walioandikishwa kama Wapiga kura kutoka katika kila mkoa kwa mikoa kumi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, miwili kati ya hiyo iwe ni ya Tanzania Visiwani.

### (ii) WAGOMBEA UBUNGE

* Sharti wateuliwe na vyama vyao vya siasa.

* Pia sharti wateuliwe na watu ishirini na tano walioandikishwa kama wapiga kura katika Jimbo linalohusika.

## KAMA WEWE UMEANDIKISHWA

* Una haki ya kumteua (kumdhamini) mgombea yeyote mmoja wa chama chochote.

* Uteuzi (udhamini) huo hufanywa kwa kutumia **"KARATASI YA UTEUZI"**.

* Haki hiyo ni kwa mgombea mmoja tu wa Urais na mmoja tu wa Ubunge. Huruhusiwi kudhamini wagombea wawili au zaidi kwa nafasi moja.

Una haki pia kuwasilisha fomu za Uteuzi za mgombea Ubunge uliyemteua (uliyemdhamini), kwa niaba yake, kwa Msimamizi wa Uchaguzi mnamo siku ya Uteuzi. Vile vile una haki ya kuwasilisha Fomu za uteuzi za mgombea Urais uliyemteua (uliyemdhamini) kwa niaba yake kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

## KAMPENI ZA UCHAGUZI

* Zitafanywa kwa njia mbali mbali na vyama vya siasa. Kwa mfano:

  - Mikutano ya hadhara.
  - Kuwatembelea wapiga kura.
  - Kubandika matangazo sehemu mbalimbali.

  Unashauriwa kuhudhuria mikutano hiyo, kuwasikiliza, na kusoma matangazo

  Unapohudhuria mkutano, au unapotembelewa ni haki yako kuuliza maswali. Lakini fanya hivyo kwa utulivu.

  Kwa kufanya hivyo utawaelewa wagombea na sera za vyama vyao. Hii itakusaidia kutumia kura yako kwa busara siku ya kupiga kura.

## UPIGAJI KURA

- Kabla ya siku ya uchaguzi nenda mahali ulipojiandikisha. Hapo utakuta tangazo linaloonyesha kituo utakapopigia kura. Tangazo hilo litawekwa angalau siku nane kabla ya siku ya upigaji kura.
- <u>Muhimu:</u> Uende hapo ukijua namba yako ya kuandikishwa. Hiyo ndiyo utakayoikuta.

## SAA ZA KUPIGA KURA

Kwa kawaida vituo hufunguliwa saa mbili asubuhi na hufungwa saa kumi na mbili jioni. Hata hivyo muda huo unaweza kubadilishwa. Mabadiliko hayo yakifanywa yatatangazwa kwenye tangazo lililotajwa hapo juu.

- Nenda na Fomu Namba 1 ambayo ulipewa siku ulipojiandikisha kuwa mpiga kura. Nenda kituoni wewe mwenyewe.
- Usiende na matangazo au kitu kingine chochote kinachoweza kuonyesha kwamba ni cha kampeni kwa mfano nguo, mabango n.k.
- Ukikuta wapiga kura wenzako wamejipanga kwenye mstari simama nyuma ya waliotangulia.
- Uwe mtulivu.
- Usipige kura kwa kushawishiwa, rushwa au kwa kutishwa.
- Kampeni ya aina yoyote hairuhusiwi hapo Kituoni. Hairuhusiwi hata kidogo

## NANI WA KUMPIGIA KURA:

**MPIGIE KURA MGOMBEA YEYOTE UNAYEMTAKA HATA KAMA SI MGOMBEA WA CHAMA CHAKO AU HATA KAMA WEWE SI MWANACHAMA WA CHAMA CHOCHOTE CHA SIASA. KURA YAKO NI SIRI YAKO**

## JINSI YA KUPIGA KURA

* Kwenye kituo cha kupigia kura kutakuwa na masanduku aina mbili. Sanduku la buluu ni kwa ajili ya kura za Rais na sanduku jeusi kwa ajili ya kura za Mbunge.

* Utawajibika kupiga kura za aina mbili, moja kwa ajili ya kumchagua Rais na ya pili kwa ajili ya kumchagua Mbunge. Karatasi hizo za kura zitakuwa na rangi tofauti.

* Mpe Msimamizi Msaidizi wa Kituo Fomu Namba 1 uliyokwenda nayo Kituoni kutoka nyumbani.

* Jina lako litasomwa kwa sauti ili mawakala wa wagombea waliopo wasikie.

* Mawakala wa Wagombea, na hata Wasimamizi wa kituo, wana haki ya kukuuliza maswali waridhike kwamba mwenye jina hilo ni wewe; na kama una sifa za kupiga kura.

**WAJIBU MASWALI YAO KWA UTULIVU**

* Nenda sehemu maalum iliyotengwa kwa kupigia kura.

* Weka alama hii [✔] NDANI ya chumba kilichopo chini ya picha ya mgombea unayetaka kumchagua.

**USIANDIKE NENO AU KUWEKA ALAMA NYINGINE YOYOTE KWENYE KARATASI YA KURA. UKIFANYA HIVYO KURA YAKO ITAKUWA IMEHARIBIKA NA HAITA HESABIWA**

* Zikunje karatasi zako vizuri kama zilivyokunjwa ulipopewa.

* Mwonyeshe Msimamizi wa kituo sehemu iliyogongwa muhuri. Kisha tumbukiza karatasi ya uchaguzi wa Bunge kwenye sanduku jeusi na ya uchaguzi wa Rais kwenye sanduku la buluu. Kabidhi kalamu ya wino kwa Msimamizi wa kituo.

**KUMBUKA KUWA KURA YAKO NI SIRI YAKO; USIMWONYESHE MTU MWINGINE AU KUTAJA MGOMBEA ULIYEMPIGIA KURA**

* Wapiga kura wasiojua kusoma na kuandika, wasiojua namna ya kupiga kura, vilema na wasioona watasaidiwa na watu watakaowateua wao wenyewe.

## KUTANGAZA MATOKEO

* Baada ya kura kuhesabiwa, matokeo ya uchaguzi wa Bunge yatatangazwa mara moja na Msimamizi wa Uchaguzi.

* Kwa Uchaguzi wa Rais, Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza kura alizopata kila mgombea bila kutaja mshindi ni nani.

* Matokeo ya Uchaguzi wa Rais yatatangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

## MAMBO AMBAYO NI UVUNJAJI WA SHERIA KWA MPIGA KURA

Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo mpiga kura akiyafanya atakuwa amevunja sheria:

* Kufanya fujo kwenye eneo la kituo cha kupigia kura.
* Kuzuia mtu kwa namna yoyote asipige kura yake.
* Kujiandikisha au kupiga kura zaidi ya mara moja.
* Kupiga kura wakati huna haki ya kufanya hivyo.
* Kupiga kura kwa kutumia jina la mtu mwingine, mtu aliyekufa au kwa kutumia jina la uongo.
* Kutumbukiza ndani ya sanduku la kura karatasi nyingine yoyote badala ya karatasi rasmi ya kura.
* Kutoa au kupokea rushwa.

**Makosa yanayokatazwa siku ya kupiga kura:**

* Kutoa karatasi yako ya kupigia kura kwa mtu mwingine.
* Kufanya kampeni siku ya kupiga kura.
* Kuvaa, au kuwa na alama ya chama cha siasa cha mgombea mmojawapo, karibu na eneo la Kituo cha Kupigia Kura.
* Kuzuia mtu kwa namna yoyote asipige kura yake.

**USIPOTEZE HAKI YAKO**

**KAJIANDIKISHE UPIGE KURA**

Country TANZANIA

Year '95 Language kiswahili

Description Instructions to voters for presidential & parliamentary elections

IFES developed/sponsored? ______

# NEW DOCUMENT

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# MAELEKEZO KWA MPIGA KURA

## UCHAGUZI

## WA

## RAIS NA WABUNGE

## 1995

# UCHAGUZI WA RAIS NA WABUNGE

# 1995

# MAELEKEZO KWA MPIGA KURA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI
S.L.P. 10923
DAR ES SALAAM

## UJUMBE WA MWENYEKITI

Tanzania ni Nchi inayofuata utaratibu wa Vyama vingi vya Siasa. Vyama vinavyoshiriki katika Uchaguzi ni vyama vilivyoandikishwa kisheria, kwa hiyo vinashiriki katika Uchaguzi huu kihalali kabisa.

Kila raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea ana haki ya kujiandikisha kuwa mpiga kura. Kukosa kupiga kura ni kujinyima haki yako. Kwa hiyo una wajibu wa kujiandikisha na kupiga kura. Jiandikishe na kupiga kura hata kama wewe si mwanachama wa chama chochote cha siasa. Kura yako ni siri yako.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inafanya kila linalowezekana ili uchaguzi uwe huru na wa haki.

**USIKOSE KUJIANDIKISHA**

**USIKOSE KUPIGA KURA**

**(Jaji Lewis M. Makame)**
**MWENYEKITI**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## UTANGULIZI

Kiti cha Rais/Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kitagombewa na wagombea watakaoteuliwa na Vyama vya Siasa vilivyopata usajili kamili. Mgombea atakayeshinda ndiye atatangazwa rasmi kuwa Rais/Makamu wa Rais kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Kiti cha Ubunge kitagombewa na wagombea wa vyama mbalimbali vya siasa. Mgombea atakayeshinda atakuwa ni Mbunge wa Jimbo lako kwa kipindi cha miaka mitano. Mbunge huyo ndiye atakaye kuwakilisha Bungeni wewe na wenzako wa Jimbo lako.

Kushiriki kwako katika chaguzi hizo ni muhimu kwako na kwa Taifa. Kutokana na umuhimu huu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa Maelekezo haya ili kukusaidia wewe na wenzako kushiriki vyema katika hatua mbalimbali za uchaguzi.

Ni matumaini yangu kwamba Maelekezo haya utayasoma na kuyazingatia.

UKISHA KUJIANDIKISHA USIKOSE KUPIGA KURA.

**(ALEX T. BANZI)**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

**KWA NINI TUNACHAGUA:**

- Tunatumia haki yetu Kikatiba.

- Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - ni Wakuu wa Nchi.

- Wabunge ndio wawakilishi wa wananchi Bungeni. Viongozi hao ni muhimu kwa kuwa ndio:-

  . Wanaohamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo yao.

  . Wanaopitisha Sheria na Sera mbali mbali kwa maendeleo ya wananchi.

**KUJIANDIKISHA KUPIGA KURA**

**KWA NINI NI MUHIMU KUJIANDIKISHA:**

- Bila kujiandikisha hutaruhusiwa kupiga kura.

- Usipopiga kura utakuwa umepoteza haki yako ya kumchagua Kiongozi anayefaa.

**LINI UKAJIANDIKISHE:**

Kwa jumla tarehe za uandikishaji wa Wapiga kura hupangwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Kwa uchaguzi wa Rais/Makamu wa Rais na Wabunge wa Mwaka 1995 uandikishaji utafanyika kuanzia tarehe 6 Agosti hadi tarehe 4 Septemba, 1995.

## WAPI UKAJIANDIKISHE:

- Ukajiandikishe katika kituo cha kujiandikisha kilichopo katika kijiji chako, au Kitongoji chako au Mtaa wako.

- Vituo nivyo vitatangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo lako kabla ya tarehe ya kuanza kujiandikisha.

- Kila mahali pa kujiandikisha patakuwa na bango lililoandikwa "KITUO CHA KUANDIKISHA WAPIGA KURA".

## MASWALI UTAKAYOULIZWA WAKATI WA KUANDIKISHWA

Ili uweze kuandikishwa Mwandishi atahitaji kufahamu, kutoka kwako, mambo yafuatayo:

- Majina yako (Jina lako, la baba yako na la ukoo).

- Uraia wako.

    * Kama wewe ni raia wa kuandikishwa, kumbuka namba yako ya kuandikishwa kuwa raia wa Tanzania.

- Umri wako.

- Mahali unapoishi, kwa kawaida.

- Kama hujaandikishwa mahali pengine popote.

**KUMBUKA KUWA TAARIFA SAHIHI NI MUHIMU ILI UWEZE KUANDIKISHWA KUWA MPIGA KURA**

**BAADA YA KUANDIKISHWA:**

- Utapewa Fomu Namba 1.

  * Ni Fomu ya Kuandikishwa kuwa Mpiga Kura. Ina namba ya kuandikishwa na tarehe uliyoandikishwa katika Jimbo linalohusika.

  * Itunze vizuri fomu hiyo. Maana ni ushahidi kwamba umeandikishwa . Siku ya kupiga kura LAZIMA uende nayo kituoni.

  * Utapewa pia karatasi yenye vidokezo muhimu kuhusu hatua mbalimbali za uchaguzi wa Rais/Makamu wa Rais na Wabunge. Kaisome vizuri.

**UKIKATALIWA KUANDIKISHWA**

* Utaelezwa sababu.

* Ukiridhika, rudi nyumbani.

  Usiporidhika, una haki ya kumwomba Mwandishi akueleze sababu hizo kwa maandishi.

* Kama bado huridhiki unaweza kumwona Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au hata Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo lako.

* Kama uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi nao hautakuridhisha una haki ya kwenda kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi. Lakini: itabidi uende kabla ya kupita siku 21 tangu siku utakapokataliwa kuandikishwa.

## FOMU NA. 2 - ORODHA YA WAPIGA KURA WALIOANDIKISHWA:

* Itakuwepo ofisini kwa Msimamizi wa Uchaguzi mara baada ya siku ya mwisho ya uandikishaji wa wapiga kura.

* Una haki ya kukagua orodha hiyo katika kipindi rasmi kitakachowekwa.

* Ukiona jina la mtu ambae una hakika amekufa au hana sifa za kuandikishwa, una haki ya kudai jina hilo lifutwe.

* Ukiona jina lako halimo na una hakika ulijiandikisha una haki ya kudai jina lako liingizwe kwenye orodha hiyo.

## SIFA ZA KUWA MPIGA KURA

- Kuwa raia wa Tanzania.

- Kuwa na umri wa miaka 18 na kuendelea.

- Kuwa mkazi wa kawaida wa eneo unapokuja kujiandikisha kuwa mpiga kura.

## LAKINI

* Hata kama mtu ana sifa hizo zilizotajwa hapo juu, hastahili kuandkishwa iwapo:-

    - ni raia wa nchi nyingine.

    amethibitishwa kisheria kwamba ni mgonjwa wa akili, ni mwendawazimu na amewekwa kizuizini kwa ajili hiyo.

    -- amewekwa kizuizini kwa amri ya Rais

- amehukumiwa kifo au anatumikia kifungo kinachozidi miezi sita.

- kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge inayoshughulikia makosa yanayohusika na uchaguzi wa aina yoyote mtu huyo amezuiliwa kujiandikisha kama mpiga kura.

## UTEUZI WA WAGOMBEA

### (i) WAGOMBEA URAIS NA MAKAMU WA RAIS

* Sharti wateuliwe na vyama vyao vya siasa.

* Pia sharti wateuliwe na watu 200 walioandikishwa kama Wapiga kura kutoka katika kila mkoa kwa mikoa kumi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, miwili kati ya hiyo iwe ni ya Tanzania Visiwani.

### (ii) WAGOMBEA UBUNGE

* Sharti wateuliwe na vyama vyao vya siasa.

* Pia sharti wateuliwe na watu ishirini na tano walioandikishwa kama wapiga kura katika Jimbo linalohusika.

## KAMA WEWE UMEANDIKISHWA

* Una haki ya kumteua (kumdhamini) mgombea yeyote mmoja wa chama chochote.

* Uteuzi (udhamini) huo hufanywa kwa kutumia "KARATASI YA UTEUZI".

* Haki hiyo ni kwa mgombea mmoja tu wa Urais na mmoja tu wa Ubunge. Huruhusiwi kudhamini wagombea wawili au zaidi kwa nafasi moja.

Una haki pia kuwasilisha fomu za Uteuzi za mgombea Ubunge uliyemteua (uliyemdhamini), kwa niaba yake, kwa Msimamizi wa Uchaguzi mnamo siku ya Uteuzi. Vile vile una haki ya kuwasilisha Fomu za uteuzi za mgombea Urais uliyemteua (uliyemdhamini) kwa niaba yake kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

## KAMPENI ZA UCHAGUZI

* Zitafanywa kwa njia mbali mbali na vyama vya siasa. Kwa mfano:
    - Mikutano ya hadhara.
    - Kuwatembelea wapiga kura.
    - Kubandika matangazo sehemu mbalimbali.
* Unashauriwa kuhudhuria mikutano hiyo, kuwasikiliza, na kusoma matangazo
* Unapohudhuria mkutano, au unapotembelewa ni haki yako kuuliza maswali. Lakini fanya hivyo kwa utulivu.
* Kwa kufanya hivyo utawaelewa wagombea na sera za vyama vyao. Hii itakusaidia kutumia kura yako kwa busara siku ya kupiga kura.

## UPIGAJI KURA

- Kabla ya siku ya uchaguzi nenda mahali ulipojiandikisha. Hapo utakuta tangazo linaloonyesha kituo utakapopigia kura. Tangazo hilo litawekwa angalau siku nane kabla ya siku ya upigaji kura.
- Muhimu: Uende hapo ukijua namba yako ya kuandikishwa. Hiyo ndiyo utakayoikuta.

## SAA ZA KUPIGA KURA

Kwa kawaida vituo hufunguliwa saa mbili asubuhi na hufungwa saa kumi na mbili jioni. Hata hivyo muda huo unaweza kubadilishwa. Mabadiliko hayo yakifanywa yatatangazwa kwenye tangazo lililotajwa hapo juu.

- Nenda na Fomu Namba 1 ambayo ulipewa siku ulipojiandikisha kuwa mpiga kura. Nenda kituoni wewe mwenyewe.

- Usiende na matangazo au kitu kingine chochote kinachoweza kuonyesha kwamba ni cha kampeni kwa mfano nguo, mabango n.k.

- Ukikuta wapiga kura wenzako wamejipanga kwenye mstari simama nyuma ya waliotangulia.

- Uwe mtulivu.

- Usipige kura kwa kushawishiwa, rushwa au kwa kutishwa.

- Kampeni ya aina yoyote hairuhusiwi hapo Kituoni. Hairuhusiwi hata kidogo.

## NANI WA KUMPIGIA KURA:

**MPIGIE KURA MGOMBEA YEYOTE UNAYEMTAKA HATA KAMA SI MGOMBEA WA CHAMA CHAKO AU HATA KAMA WEWE SI MWANACHAMA WA CHAMA CHOCHOTE CHA SIASA. KURA YAKO NI SIRI YAKO**

## JINSI YA KUPIGA KURA

* Kwenye kituo cha kupigia kura kutakuwa na masanduku aina mbili. Sanduku la buluu ni kwa ajili ya kura za Rais na sanduku jeusi kwa ajili ya kura za Mbunge.

* Utawajibika kupiga kura za aina mbili, moja kwa ajili ya kumchagua Rais na ya pili kwa ajili ya kumchagua Mbunge. Karatasi hizo za kura zitakuwa na rangi tofauti.

* Mpe Msimamizi Msaidizi wa Kituo Fomu Namba 1 uliyokwenda nayo Kituoni kutoka nyumbani.

* Jina lako litasomwa kwa sauti ili mawakala wa wagombea waliopo wasikie.

* Mawakala wa Wagombea, na hata Wasimamizi wa kituo, wana haki ya kukuuliza maswali waridhike kwamba mwenye jina hilo ni wewe; na kama una sifa za kupiga kura.

**WAJIBU MASWALI YAO KWA UTULIVU**

* Nenda sehemu maalum iliyotengwa kwa kupigia kura.

* Weka alama hii [✔] NDANI ya chumba kilichopo chini ya picha ya mgombea unayetaka kumchagua.

**USIANDIKE NENO AU KUWEKA ALAMA NYINGINE YOYOTE KWENYE KARATASI YA KURA. UKIFANYA HIVYO KURA YAKO ITAKUWA IMEHARIBIKA NA HAITA HESABIWA**

* Zikunje karatasi zako vizuri kama zilivyokunjwa ulipopewa.

* Mwonyeshe Msimamizi wa kituo sehemu iliyogongwa muhuri. Kisha tumbukiza karatasi ya uchaguzi wa Bunge kwenye sanduku jeusi na ya uchaguzi wa Rais kwenye sanduku la buluu. Kabidhi kalamu ya wino kwa Msimamizi wa kituo.

**KUMBUKA KUWA KURA YAKO NI SIRI YAKO; USIMWONYESHE MTU MWINGINE AU KUTAJA MGOMBEA ULIYEMPIGIA KURA**

* Wapiga kura wasiojua kusoma na kuandika, wasiojua namna ya kupiga kura, vilema na wasioona watasaidiwa na watu watakaowateua wao wenyewe.

## KUTANGAZA MATOKEO

* Baada ya kura kuhesabiwa, matokeo ya uchaguzi wa Bunge yatatangazwa mara moja na Msimamizi wa Uchaguzi.

* Kwa Uchaguzi wa Rais, Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza kura alizopata kila mgombea bila kutaja mshindi ni nani.

* Matokeo ya Uchaguzi wa Rais yatatangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

## MAMBO AMBAYO NI UVUNJAJI WA SHERIA KWA MPIGA KURA

Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo mpiga kura akiyafanya atakuwa amevunja sheria:-

* Kufanya fujo kwenye eneo la kituo cha kupigia kura.
* Kuzuia mtu kwa namna yoyote asipige kura yake.
* Kujiandikisha au kupiga kura zaidi ya mara moja.
* Kupiga kura wakati huna haki ya kufanya hivyo.
* Kupiga kura kwa kutumia jina la mtu mwingine, mtu aliyekufa au kwa kutumia jina la uongo.
* Kutumbukiza ndani ya sanduku la kura karatasi nyingine yoyote badala ya karatasi rasmi ya kura.
* Kutoa au kupokea rushwa.

**Makosa yanayokatazwa siku ya kupiga kura:-**

* Kutoa karatasi yako ya kupigia kura kwa mtu mwingine.
* Kufanya kampeni siku ya kupiga kura.
* Kuvaa, au kuwa na alama ya chama cha siasa cha mgombea mmojawapo, karibu na eneo la Kituo cha Kupigia Kura.
* Kuzuia mtu kwa namna yoyote asipige kura yake.

**USIPOTEZE HAKI YAKO**
**KAJIANDIKISHE UPIGE KURA.**

Country ______
Year ______ Language ______
Description ______
______
______
______
IFES developed/sponsored? ______